## MAJUKUMU MAKUU YA BARAZA

Kwa mujibu wa Sheria hiyo majukumu ya Baraza ni:

- Kutekeleza shughuli za Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira (Enforcement and Compliance);
- Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM);
- Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya maamuzi yanayohusu mazingira; na
- Kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira.

## MAJUKUMU MENGINE YA BARAZA

Kifungu Na.18 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 ya Mwaka 2004 kimeanisha majukumu ya Baraza kama ifuatavyo: -

a. Kufanya uhakiki wa mazingira (Environmental Audit);

b. Kufanya tathmini ambazo zitasaidia katika kuhifadhi na kusimamia Mazingira;

c. Kufanya utafiti na kuratibu utafiti wa mazingira, kuchunguza, kutathmini na kukusanya taarifa na matokeo ya utafiti na kuzisambaza kwa wadau;

d. Kufanya mapitio na kutoa mapendekezo ili kuwezesha kupitishwa kwa taarifa/ripoti za TAM;

e. Kuainisha miradi au programu zinazohitaji kufanyiwa ukaguzi na ufuatiliaji (Audit and Monitoring);

f. Kuhimiza na kuhakikisha usimamizi na uzingatiaji wa viwango vya taifa katika utekelezaji wa Sheria;

g. Kuanzisha hatua madhubuti zenye lengo la kulinda na kudhibiti ajali zinazoweza kusababisha uharibifu wa mazingira na kubuni njia za kurekebisha maeneo ambayo yamepata uharibifu;

h. Kutekeleza programu zenye lengo la kutoa elimu ya mazingira na kukuza weledi kwa kushirikiana na taasisi na sekta za wizara mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha usimamizi madhubuti na ushiriki wa jamii unafanywa katika shughuli za kuhifadhi mazingira;

i. Kuchapisha na kusambaza miongozo mbalimbali ya usimamizi wa mazingira inayolenga kuhakikisha udhibiti wa uharibifu wa mazingira unafanyika;

j. Kutoa ushauri wa kitaalam na kusaidia taasisi na asasi mbalimbali zinazoshughulika na usimamizi wa maliasili na mazingira; na

k. Kufanya shughuli nyingine zozote kwa maagizo ya Waziri wa Mazingira au kutokana na uhitaji wakati wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

## DIRA NA DHIMA

- **DIRA:** Kuwa Taasisi yenye hadhi ya kimataifa inayosimaimia hifadhi ya mazingira kwa kuhakikisha kuwa mazingira yanakuwa bora kwa ajili ya watu na viumbe wengine.
- **DHIMA:** Kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa kupitia uratibu, uwezeshaji, kutoa elimu, usimamizi wa Sheria, ufuatiliaji na utafiti wa mazingira.

## HUDUMA ZETU

**Baraza liinatoa huduma zifuatazo:**

- Ukaguzi wa mazingira
- Usajili wataalamu elekezi wa mazingira
- Uendeshaji wa tafiti za mazingira
- Elimu ya mazingira, mipango ya utekelezaji na ufuatailiaji masharti.



*Tukitunza mazingira tunatunza uwepo wa maisha yetu sisi wenyewe*

## KURUGENZI NA VITENGO

- **Kurugenzi ya Uzingatiaji na Utekelezaji wa Mazingira (DECE)**

  Kusimamia uzingatiaji wa Sheria, kufanya ukaguzi na kufuatilia utekelezaji wa Sheria

- **Kurugenzi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (DESIA)**

  Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika miradi mipya na inayoendelea.

- **Kurugenzi ya Utafiti na Usimamizi wa Mazingira (DERM)**

  Kuratibu na kuelekeza utekelezaji wa Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mazingira (RERA), Usimamizi wa Mifumo ya Kiikolojia na masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi.

- **Kurugenzi ya Fedha na Utawala**

  Usimamizi wa fedha, rasilimali watu na masuala ya utawala na vifaa.

- **Kitengo cha Huduma za Kisheria**

  Kutoa utaalamu na huduma katika masuala ya kisheria

- **Kitengo cha Ukaguzi wa ndani**

  Kutoa huduma za ushauri kwa Afisa Masuuli katika usimamizi mzuri wa rasilimali za Baraza.

- **Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

  Kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na masuala yote yanayohusu Baraza na kujenga uelewa kwa jamii kuhusu usimamizi, utunzaji na uhifadhi wa Mazingira. Aidha Kitengo hurahisisha mtiririko wa taarifa kwenda kwa jamii na kupata mrejesho toka kwa jamii.

- **Kitengo cha TEHAMA na Takwimu**

  Kutoa ushauri na utaalam juu ya maendeleo na utumiaji wa teknolojia katika utoaji huduma bora na uchambuzi wa takwimu.

- **Kitengo cha Ununuzi na Ugavi**

  Kutoa utaalamu juu ya usimamizi wa michakato ya manunuzi na kusimamia shughuli zote za zabuni za Baraza.

- **Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini**

  Kuratibu uundaji wa mipango ya ushirika na kusimamia utekelezaji wake.

**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA LINA MAKAO YAKE MAKUU JIJINI DODOMA NA OFISI 13 ZA KANDA**

| Na. | MAKAO MAKUU | ANUANI |
|---|---|---|
| | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) | Mkurugenzi Mkuu,<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC)<br>Kambarage Tower, Ghorofa ya 6<br>P.O.Box 2724, Dodoma Tanzania<br>Simu: +255 26 2960098, +255 713 608 930<br>Nukushi: +255 22 2774901<br>WhatsApp: +255 737 796 252<br>Tovuti: www.nemc.or.tz<br>Barua pepe: dg@nemc.or.tz |
| | **OFISI ZA KANDA** | |
| 1 | Kanda ya Ziwa inayohusisha Mikoa ya Mwanza ,Simiyu, Mara, Shinyanga na Geita.<br>Ofisi zake ziko | PSSSF Front Wing, 6th Floor, Plot No. 17/1, 17/2 and 18, Barabara ya Kenyata,<br>P.O. Box 11045, Mwanza<br>Phone. 0782296112, 0713296112 |
| 2 | Kanda ya Kaskazini inayohusisha Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.<br>Ofisi zake ziko Mkoa wa Arusha Mkoa wa Mwanza. | Makutano ya Makongoro-Goliondoi, Mzunguko wa Ngorongoro, Kitalu Na. 055019/1 and 055019/6, Jengo la utalii la Ngorongoro, Ghorofa 6<br>S.L.P 1041 Arusha<br>Simu: +255738064966, 0784333583, 0655333538<br>Barua pepe:<br>nemcarusha@nemc.or.tz |
| 3 | Kanda ya Nyanda za juu Kusini inayohusisha Mikoa ya (Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe).<br>Ofisi zake ziko Mkoa wa Mbeya | Karume Avenue,<br>S.L.P 6215, Mbeya,<br>Telephone 0713390379<br>Barua pepe:<br>nemcmbeya@nemc.or.tz |
| 4 | Kanda ya Kati inayohusisha Mikoa ya Dodoma, Tabora na Singida. Ofisi zake ziko Mkoa wa Dodoma | Jengo la PSPF Dodoma Plaza, Ghorofa ya 6<br>S.L.P 2724, Dodoma.<br>Simu. +255262963859/860<br>Barua pepe:<br>nemcdodoma@nemc.or.tz |
| 5 | Kanda ya Kusini Mtwa inayohusisha Mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Lindi . | Raha leo Complex (Jengo la NHC, Ghorofa 3)<br>S.L.P 1259, Mtwara.<br>Simu. +255232334683, 0767153776, 0621989301<br>Barua pepe.<br>nemcmtwara@nemc.or.tz |
| 6 | Kanda ya Magharibi inayohusisha Mikoa ya (Kigoma, Katavi, Tabora na Kagera )<br>Ofisi zake zipo Kigoma | Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya 1, Kitalu Na. 100 Nyumba na 1, Mtaa wa Mnarani.<br>P.O. Box 974, Kigoma Ujiji.<br>Simu.0713566367<br>Barua pepe:<br>nemckigoma@nemc.or.tz |
| 7 | Kanda ya Mashariki Kusini inayohusisha Mkoa wa Dar es salaam, wilaya ya Mkuranga, Kigamboni, Mafia, Kisarawe na Kibiti | Mtaa wa Regent. Kitalu No. 28-30,<br>S.L.P 63154<br>Simu. +25522 277 4889, 0756664775<br>Dar es salaam Tanzania |
| 8 | Kanda ya Mashariki Kaskazini inayohusisha Wilaya ya (Kinondoni, Ubungo and Kibaha). Ofizi zake ziko Mkoa wa Dar es salaam | Regent St. Kitalu No. 28-30,<br>S.L.P 63154<br>Simu. +25522 277 4889, 0742 774735<br>Dar es salaam Tanzania |
| 9 | Kanda ya Morogoro Rufiji | S.L.P 1342, Morogoro<br>Simu: 0784 506267/<br>0738 953787<br>Barua Pepe:<br>nemcmorogoro@nemc.or.tz |
| 10 | Kanda ya Ilala | Regent St. Plot No. 28-30,<br>S. L. P 63154<br>Simu. +25522 277 4889, 07846303539.<br>Dar es salaam Tanzania |
| 11 | Kanda ya Temeke | Regent St. Kitalu No. 28-30,<br>S.L.P 63154<br>Simu. +25522 277 4889,0676 164088<br>Dar es salaam Tanzania |
| 12 | Kanda ya Bagamoyo inayohusisha Mkoa wa Tanga pamoja na Wilaya ya Bagamoyo | Regent St. Plot No. 28-30,<br>S.L.P 63154<br>Simu.+25522 277 4889, 0753402334<br>Dar es salaam Tanzania |
| 13 | Kanda ya ziwa Victoria Magharibi. | Ofisi zake zipo Geita<br>Simu: 0685 117589 |


**Mkurugenzi Mkuu**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**
Kambarage Tower, 6th Floor
P.O Box 2724, Dodoma,Tanzania,
Tel: +255 26 2960 098, +255 713 608 930,
Nukushi: +255 22 277 4901, Whatsap: +255 737 796 252
Email: dg@nemc.or.tz | Website: www.nemc.or.tz

@nemctanzania www.nemc.or.tz

Namba ya dharura: 0800110116 NEMCTVTanzania


**#MazingiraYetuUhaiWetu**




## Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

# Kuhusu Sisi

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa Mwaka 1983 wakati Serikali ya Tanzania ilipotunga Sheria ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira Kifungu namba 19 ya mwaka 1983. Baraza lilianzishwa kutokana na uhitaji wa Kitaifa kama Taasisi katika kusimamia masuala ya utunziji wa Mazingira pamoja na utekelezaji wa maadhimio ya mkutano wa Stockholm ( 1972), ambayo ilitaka Mataifa yote kuanzisha na kuimarisha Mabaraza ya Kimataifa ya Mazingira ili kuweza kushauri Serikali na jamii ya Kimataifa katika masuala ya mazingira.Tanzania ilitekeleza mchakato huu wa Mazingira wa Ulimwengu kwa kutunga Sheria ya Mazingira ya Mwaka 1983, na kuunda Baraza la Mazingira linalojulikana kama Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambalo lilianza kufanya kazi Mwaka 1983, na uundaji na upitishwaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sheria ya Mazingira ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004. Lengo kuu la kuanzishwa kwa **Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni kusimamia Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira.**